Matatizo gani? Vipi kama kutatokea matatizo?

Malalamiko

Kama una wasiwasi kuhusu jambo lolote katika utafiti huu, usisite kumuuliza muuguzi mtafiti au daktari atakayekuhudumia, ambaye atakuwa tayari wakati wote kukupa majibu. Tumeweka namba za simu kwenye kipeperushi hiki. Kama hutaridhika na majibu yao, bado una nafasi ya kufanya hivyo. Utatakiwa kuwasiliana na kamati ya maadili (kwa kupiga simu moja kwa moja) ambayo ndio imetoa idhini ya kufanyika kwa utafiti huu. Utaweza pia kupiga simu moja kwa moja kwa mtafiti mkuu. Unayo haki hii hata kama utakuwa umeghairi kushiriki utafiti huu.

Athari

Mdhamini wa utafiti huu (Chuo kikuu cha Birmingham) na taasisi zinazofanya utafiti huu wameweka utaratibu kuhusu utafiti huu. Kama utapata athari yeyote, utastahili kupata huduma ya bima. Kama utapata madhara kutokana na uzembe wa mfanyakazi/mhudumu, unao uwezo wa kutafuta msaada wa kisheria. Tafadhali wasiliaana na mtafiti mkuu kukupatia maelezo zaidi.

Je kushiriki kwangu itakuwa siri?

Ndiyo. Taarifa zote zitakazokusanywa zitakuwa za siri. Taarifa zozote zitakazopelekwa nje ya hospitali au kupelekwa chuo kikuu cha Birmingham zitaondolewa alama za utambulisho kama jina, anwani umri ili zisiweze kutambulikana. Taarifa zote zitatunzwa kwa usiri mkubwa. Ili kuhakikisha kuwa taarifa hizi ni siri, watafiti watatumia neno la siri watakapoingia katika mafaili ya kumbukumbu (database). Hutaweza kutambuliwa binafsi kwenye majarida au machapisho yeyote yatakayotokana na utafiti huu. Wakati mwingine, utafiti huu unafuatiliwa na kuangaliwa kwamba washiriki wa utafiti wamekubali kushiriki au la.

Je majibu ya utafiti huu yatafanyiwa nini?

Mara baada ya matokeo ya utafiti huu kutolewa, yatazungumzwa kwenye mikutano mbalimbali hapa nchini na nje ya nchi. Matokeo haya pia yatachapishwa katika majarida mbalimbali hapa nchini na nje ya nchi. Pia, matokeo haya yatawekwa kweye tovuti yetu (www.aimstrial.org).

Nani ameangalia na kuidhinisha utafiti huu

Utafiti huu umepitiwa na kuidhinishwa na kamati ya maadili ya Taifa pamoja na Taasisi ya Afya ya Ifakara. Hawa ni watu ambao wamepewa kazi ya kuhakikisha kuwa tafiti zote nchini zinafikia vigezo ambavyo vinakubalika ili kuhakikisha usalama wa washiriki.

Je una maswali mengine?

Ni mategemeo yetu kuwa utakubali kushiriki kwenye utafiti huu ukishasoma kipeperushi hiki na kuzungumza na mtafiti. Iwapo una maswali kwa sasa hivi au baadae tafadhali usisite kutuuliza. Namba zetu za simu zipo chini ya kipeperushi hiki.

Utapewa nakala ya kipeperushi pamoja na fomu ya idhini kwa kumbukumbu yako.

Ahsante sana kwa muda wako wa kusoma au kusomewa kipeperushi hiki na kufikiria kujiunga na utafiti huu.

Jinsi ya kuwasiliana nasi.

Tafadhali wasiliana nasi muda wowote, mchana au usiku kwa namba ifuatayo: 0784 442491 au 0655 764647 au 0686 312214.

Tutakupatia vocha ili iwe rahisi kuwasiliana na sisi kiurahisi iwapo utakuwa na tatizo au swali lolote usisite kuuliza.

Tutakurudishia gharama zako za usafiri utakazotumia kuja hospitalini baada ya wiki mbili na iwapo utataka kuja hospitali kabla ya hapo.

Tutawasiliana ili kujua kama kuna tatizo na kukumbusha kuhusu ufuatiliaji. Vilevile tutawasiliana na wewe iwapo hatutakuona katika ufuatiliaji ili kujua kuwa unaendelea vizuri. Tutakubaliana na wewe ili kujua ni namna gani ya kuwasiliana hapo baadae.

Kwa mawasiliano zaidi:

Jina : **Dr Chibwana namba ya simu: 0655764647 au Dr Sanga namba ya simu: 0784 442491**

Tunakushukuru kwa kupata muda wa kusoma na kufikiria kushiriki katika utafiti huu.

IFAKARA HEALTH INSTITUTE
research | training | services

Version 1.0 Swahili dated 21/03/2013

AIMS

IFAKARA HEALTH INSTITUTE
research | training | services

UTAFITI KUHUSU UTUMIAJI WA DAWA ZA KUZUIA MAAMBUKIZI KWA AKINA MAMA WALIOSAFISHWA KIZAZI BAADA YA KUHARIBIKIWA NA MIMBA

Tunapenda kukukaribisha katika utafiti huu. Uko huru kuamua kushiriki au kutoshiriki. Kabla hujaamua, tungependa kukupa taarifa kamili ya madhumuni ya utafiti huu na mambo muhimu yatakayokuhusu wewe binafsi.

Lengo la utafiti huu ni kuangalia kama utumiaji wa dawa za kuzuia maambukizi zina umuhimu wa kutolewa kwa akina mama wote walioharibikiwa na mimba kabla ya kusafishwa.

Tafadhali usisite kuuliza swali lolote endapo utahitaji maelezo zaidi.

Utafiti huu umedhaminiwa na chuo kikuu cha Birmingham cha Uingereza. Utafiti huu unafadhiliwa na Jumuiya ya Tafiti za Afya, Uingereza, The Wellcome Trust na Idara ya Maendeleo ya Kimataifa, Uingereza.

UNIVERSITY OF BIRMINGHAM

SAMPLE

MAJUMUISHO

Maambukizi baada ya kusafishwa kwa kizazi yanaweza kuwa na madhara ya kiafya endapo yatadumu kwa muda mrefu.

Inafahamika kuwa baadhi ya aina za usafishaji wa kizazi unatumia dawa za kuzuia maambukizi kabla ya usafishaji unaweza kupunguza athari hizi. Lakini, hatuna uhakika kama kwa suala la kutumia dawa za maambukizi kabla ya kusafishwa kizazi (baada ya kuharibika kwa mimba) lina faida au la. Hivyo, utafiti huu utajaribu kujibu swali hili.

Tungependa kuwaomba akina mama walioharibikiwa mimba na kutaka kusafishwa kizazi kushiriki utafiti huu. Nusu ya akina mama watakaosafishwa kizazi masaa mawili kabla ya upasuaji watapatiwa dozi moja ya dawa za aina mbili kwa pamoja (Doxycycline na Metronidazole). Nusu ya akina mama wengine watapatiwa vidonge ambavyo havina dawa lakini vinafanana na dawa hizo.

Ukikubali kushiriki, tutapenda tena kukuona baada ya wiki mbili za kusafishwa kizazi. Lakini, unaweza kuja kutuona au kutupigia simu wakati wowote utakapoona dalili za matatizo au shida yeyote

Kwa mawasiliano zaidi:
Jina : Dr Chibwana namba ya simu: 0655764647 au Dr Sanga namba ya simu: 0784 442491
Tunakushukuru kwa kupata muda wa kusoma na kufikiria kushiriki katika utafiti huu.

Sababu kuu za utafiti huu

Sababu kuu ya huu utafiti ni kutaka kujua kuwa matumizi ya dawa za kuzua maambukizi kabla ya kusafishwa kizazi (baada ya kuharibika kwa mimba) inapunguza maambukizi au la. Dawa hizo ni Metronidazole 400mg na Doxycycline 400mg.

Kwa nini nimeombwa kushiriki?

Unaombwa kushiriki katika utafiti huu kwa sababu wewe ni mmojawapo uliyepata tatizo la kuharibika kwa mimba changa na unahitaji matibabu ya kusafishwa kizazi.

Je, ni lazima kushiriki?

Hapana. Upo huru kushiriki au kutoshiriki katika utafiti huu. Iwapo utakubali, utapewa kipeperushi hiki chenye hii taarifa ambacho utakisoma na kukaa nacho na utatakiwa utoe idhini kwa kusaini fomu ya ridhaa. Pia uko huru kujitoa kwenye utafiti huu wakati wowote bila kutoa sababu yeyote. Iwapo utaamua kutoshiriki au kujitoa, hakutoathiri ufuatiliaji wako wa kupatiwa matibabu kwa njia moja au nyingine.

Itakuwaje kama nikiwa mshiriki?

Ikiwa utaamua kushiriki, na umetoa ridhaa kwa kuweka sahihi kwenye fomu ya idhini, mtafiti/mtoa huduma atakupatia dawa hizo masaa mawili (2) kabla ya kusafishwa kizazi. Dawa zote zinafanana hivyo wewe au mtafiti/mtoa huduma hataweza kuzitambua hadi mwisho wa utafiti. Utapewa jumla ya vidonge vitano (5) ambavyo utatakiwa kuvimeza na maji.

Halafu utasafishwa kizazi kama ulivyopangiwa (ikiwa hakuna sababu nyingine za kutofanyiwa). Kukubali kwako kushiriki katika utafiti huu hakutabadili shughuli ya usafishwaji inayotolewa kwa akina mama walioharibikiwa mimba.

Tafadhali mweleze daktari au muuguzi atakayekushughulikia iwapo utakuwa na tatizo lolote kabla ya kuruhusiwa kwenda nyumbani. Na iwapo utakuwa na tatizo lolote ndani ya wiki mbili baada ya kuruhusiwa kutoka hospitalini, utujulishe haraka iwezekanavyo ili tuweze kukuona. Tumeweka namba ya simu kwenye kipeperushi hiki hapo chini ambayo unaweza kuitumia.

Hata kama utakuwa hujapata tatizo au shida yeyote, tunahitaji kukuona tena wiki ya pili (2) baada ya kusafishwa kizazi, ambapo utapimwa na kuchukuliwa sampuli ya damu ili kuona kama una maambukizo au la. Kama utakuwa na uambukizo, tutachukua vipimo zaidi na tutahakikisha kuwa unapata matibabu yanayostahili.

Je, nitafanya nini baada ya kusafishwa?

Tafadhali tuarifu kama utaona dalili zifuatazo baada ya siku 14 ya kusafishwa kizazi:

- Maumivu ya tumbo chini ya kinena
- Kujisikia homa au baridi na kutetetemeka
- Kutokwa na uchafu ukeni, hususani unatoa harufu mbaya
- Kutokwa na damu kwa wingi au mabonge ya damu
- Kutojisikia vizuri
- Ukiona upele au uvimbe sehemu yoyote mwilini
- Jambo jingine lolote linalokutia wasiwasi

Ni dawa gani zinazofanyiwa utafiti?

Dawa zinazofanyiwa utafiti huu ni Doxycycline na Metronidazole. Hizi ni dawa za kawaida ambazo zinatumika mahospitalini kwa kutibu masuala ya uambukizo na pia hutumiwa baada ya kusafishwa kizazi. Ni dawa za kawaida ambazo hazina athari kubwa.

Ni hasara gani nitakazoweza kupata kwa kushiriki?

Unaweza kupata athari ndogo za dawa za Doxcycline au Metronidazole, lakini huwa ni nadra sana. Kama utaona dalili zozote ambazo unadhani zinatokana na matibabu utakayopatiwa, tafadhali mwarifu daktari au muuguzi anayekuhudumia haraka iwezekanavyo.

Ni faida zipi za kushiriki utafiti huu?

Hakuna faida binafsi ya moja kwa moja ya utafiti huu, lakini, utasaidia matibabu ya watu wengi baadae. Ila, ikiwa utashiriki, tutafuatilia afya yako kwa ukaribu zaidi na kuhakikisha kuwa unapata matibabu sahihi mara tu yakitokea matatizo.

SAMPLE